# Tayarisha familia yako kwa kutolewa

get ready QUEENSLAND

Queensland Government

**Tunafurahia hali nzuri ya hewa na ya maisha hapa Queensland. Hata hivyo, maafa ya kimaumbile kama vile tufani, dhoruba, na mafuriko ni sehemu isiyozuilika katika mazingira yetu. Historia imeonyesha kwamba hatuwezi kupuulizia mbali hatari ambazo zinaletwa na haya majanga.**

Chukua muda sasa ili ujitayarishe kwa dharura kwa:

- Kutayarisha Mpango wako wa Dharua;
- Kutayarisha Mkoba wako wa Dharura,
- Kutayarisha nyumbani pako; na
- Kutega masikio endapo kutakuwa na onyo

Kazi hizi rahisi zinaweza kukusaidia kujitayarisha, kuokoka, na hata kupunguza athari ya majanga ya kimaumbile.

Kama unaishi katika eneo linalo kuelekea na mafuriko au dhoruba kali, kujipangia kutolewa sasa hivi kunaweza kukuokoa muda na unyongonyevu endapo kutakuwa na dharura kama hii.

Zifuatazo ni hatua tatu za kukusaidia kutayarisha mipangilio ya kutolewa katika Mpango wako wa Dharura.

**1. Utafiti mahitaji ya kutolewa**

- Je, nyumbani mwako pako katika eneo ambalo kuelekea na mafuriko, dhoruba kali au tsunami?
    - Angalia katika maktaba yalio karibu nawe na baraza kwa taarifa kuhusu hatari hizi zinazowezekana.
    - Angalia kwenye baraza lilio karibu nawe kuhusu mifumo ya onyo, mchakato wa kutolewa na njia zilizoteuliwa za kutolewa.
- Ni msaada upi unaopatikana kwako na familia yako endapo kutakuwa na dharura?
    - Ulizia au tafuta maelezo ya mawasiliano za wakala wa msaada walio karibu nawe.
    - Kama familia yako itahitaji msaada wa kutolewa, chunguza ni msaada upi unaopatikana kutoka kwenye baraza lililo karibu nawe na wakala wa msaada.
    - Amua namna utakavyowachunga wanyama wapenzi kama hutaweza kuandamana nao.

**2. Rekodi maelezo ya kutolewa kwenye Mpango wako wa Dharura wa Familia**

- Tambua mahali salama pa kufanya kutolewa kama dhoruba kali au mafuriko yataanza kutishia.
    - Familia au rafiki wanaoishi katika mahali salama palipo barani mbali zaidi na hatari au kwenye sehemu ya juu zaidi ndio chaguo bora zaidi.
    - Rekodi maelezo ya mawasiliano na mahali pa machaguo yako ya kuondokea kwenye Mpango wako wa Dharura.
- Tambua na andika kazi zote zinazohitajika kabla ya kutolewa na uhakikishe kwamba wanafamilia wote wanajua namna ambavyo wanaweza kukamilisha kila kazi (k.m kuhifadhi vitu vya elektroniki juu ya ardhi, kuyafunga maji, kuzima umeme na kufunga gesi katika swichi zake, na kuweka mabegi ya mchanga huko mifereji)

**3. Hakikisha kwamba familia yako imejitayarisha na inaendelea kuwa na ufahamu**

- Andaa orodha ya vitu ya kibinafsi na familia na kubeba kwenye Mkoba wako wa Kutolewa (angalia upande huu mwingine kwa yaliyomo kwenye Mkoba wa Kutolewa yaliyopendekezwa)
- Hakikisha na ufanyie mazoezi Mpango wako wa Dharura mara kwa mara (mara tatu kwa mwaka) ili kuhakikisha kwamba kila mmoja amezoea yanayohitajika katika kazi za kutolewa.
- Hakikisha ya kwamba unayo mafuta yaliyohifadhiwa salama kwenye gereji yako endapo utahitaji kutolewa kwa arifa ya haraka.
- Sikiliza matangazo ya usalama katika eneo unaloishi (kwenye redio na televisheni) ili kutambua njia za kupendelewa za kutolewa kutoka kwenye eneo lako.
- Saidia rafiki na jirani zako, haswa wazee na wale wanaohitaji msaada maalum, kwa kuwasaidia kutayarisha na kupashana habari za onyo.
- Kama unatembelea au uko kwenye likizo mjini Queensland, au kwa jimbo lingine, na huna familia au rafiki wowote kukaa nao, wasiliana na msimamizi wako wa malazi ili kutambua machambuo yaliyopo ya kutolewa.

**Orodha ya Kutolewa**

- ☐ Je, ushauri rasmi umetolewa kwa watu kutolewa?
- ☐ Je, unajua pale utakapokuwa kutolewa hadi?
- ☐ Je, sehemu yako ya kutolewa imo ndani zaidi, au juu zaidi ya ardhi na iko salama?
- ☐ Je, unajua njia ya kupendelewa ya kutolewa?
- ☐ Je, gari lako linayojaa na mafuta?
- ☐ Je, umetayarisha Mkoba wako wa Kutolewa?
- ☐ Je, umejumuisha Mkoba wako wa Kutolewa pamoja na nakala ya Mpango wako wa Dharura?
- ☐ Je, unazo dawa zinazohitajika kwa familia yako?
- ☐ Je, umefunga nyaraka na vitu vyako vya muhimu?
- ☐ Je, umezima umeme, ukafunga gesi na swichi kuu za maji katika nyumba yako?
- ☐ Je, wanyama wapenzi wako salama na imesalimishwa?
- ☐ Je, umesalimisha na kufunga nyumbani pako?
- ☐ Je, umefunga akiba ya maji unayohitaji kwa dharura?
- ☐ Je, umeangalia jirani walio wazee au walemavu?
- ☐ Kama umekamilisha vitu vyote vilivyotajwa hapo juu, basi hakikisha kwamba unavyo Mkoba wako wa Dharura na Mkoba wako wa Kutolewa na uanze Mpango wako wa Kutolewa.

## siku zote kumbuka

**Kuwa na Mpango wa Dharura ni hatua muhimu kwa familia yako katika kutayarisha, kuishi na kustahimili dharura.**

**Wanafamilia wote wanahitaji kujua pale ambapo Mpango wako wa Dharura unawekwa.**

**Fanya mazoezi kuhusu Mpango wako wa Dharura na mipangilio yako ya kutolewa kila baada ya miezi michache ili kuhakikisha kwamba kila mtu anajua cha kufanya endapo dharura itatokea.**

# Mkoba wa Kutolewa

**Mkoba wako wa Kutolewa unafaa kuhifadhiwa kwenye sanduku au begi la kuhifadhi dhabiti, rahisi kubeba au lisilopitisha maji na kuhifadhiwa mahali salama ambapo ni rahisi kufikiwa.**

**Mkoba wako wa Kutolewa umeundwa kuwa nyongeza ya Mkoba wako wa Dharura. Kama utatolewa, wakati unaamilisha Mpango wako wa Dharura basi beba Mkoba wako wa Dharura, Mpango wako wa Dharura, na Mkoba wako wa Kutolewa pamoja nawe.**

**Vitu vya kujumuisha katika Mkoba wako wa Kutolewa**

- Nguo mbalimbali za kubadilisha kwa wanafamilia, zilizohifadhiwa katika mabegi ya plastiki yasiyopitisha maji (kaptura ndefu, mashati yenye mikono mirefu, kofia na viatu dhabiti vinapendekezwa)
- Dawa muhimu za ziada na dawa zilizoshauriwa na daktari
- Nyenzo za ziada za Huduma ya Kwanza, miwani ya kuzuia jua, na vifukuza wadudu
- Vitu vya kujikwatua na vya usafi
- Mito, mabegi ya kulalia na mablanketi kwa kila mwanafamilia
- Vitabu na michezo kwa watoto
- Fomula ya ziada ya mtoto, chakula na nepi (kama zitahitajika)
- Vitu vya thamani, picha (zilizochapishwa, diski za santuri, diski mwake ya USB) na vikumbusho katika begi ya plastiki yasiyopitisha maji
- Pesa za ziada zikiwa taslimu
- Simu ya mkononi, betri ya ziada na chaja

**Nyaraka muhimu**

- Weka nakala zako asilia au idhinishwa za nyaraka zifuatazo kwenye Mkoba wako wa Dharura na Mkoba wako wa Kutolewa.
- Nakala za nyaraka hizi zilizoskaniwa na kuhifadhiwa kwenye diski mwake ya USB au CD inayojumuisha zote hizi katika mkoba wako vile vile. Weka vitu vyote hivi kwenye mabegi ya plastiki yaliofungwa.

☐ Karatasi za bima za nyumba na yaliyomo

☐ Karatasi za bima za magari na vitu vya thamani

☐ Orodha ya bidhaa za thamani za nyumbani

☐ Nyaraka za wosia na bima ya maisha

☐ Nyaraka za vyeti vya umiliki wa nyumba/ rehani yake

☐ Vyeti vya kuzaliwa na ndoa

☐ Pasipoti/maelezo ya visa

☐ Hisa na bondi

☐ Kadi za matibabu na malipo ya pensheni

☐ Kumbukumbu za chanjo


☐ Maelezo ya akaunti ya benki na kadi ya mkopo

☐ Nakala chelezo za faili muhimu za kompyuta

☐ Nakala ya Mpango wa Dharura wa nyumbani

☐ Nambari za simu za mawasiliano ya dharura

## Mkoba wa Kutolewa




*Broshua hii ni ya taarifa pekee na inatolewa kwa roho safi. Idara ya Usalama wa Jumuia, Usimamizi wa Dharura wa Queensland na Huduma ya Dharura ya Serikali yote haitawajibikia mtu yeyote kwa mujibu wa kupoteza au kuharibika kokote (kukiwemo athari ya kupoteza au kuharibu) ambayo kunaweza kupatikana au kutozwa, au kunakoweza kutokea moja kwa moja au vinginevyo, kwa mujibu wa kutegemea wa mtu yeyote katika taarifa ilimo kwenye broshua hii.*

© 2013 Department of Community Safety

*Kwa taarifa zaidi kuhusu kujitayarishia kupatwa na dharura **tembelea www.disaster.qld.gov.au***



Queensland Government